**TANGAZO LA SERIKALI NA………LA TAREHE …………**

**SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA SURA YA 290**

**SHERIA NDOGO**

***Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 7(1) (y) na 16 (1)***

**SHERIA NDOGO YA (USHURU WA HUDUMA) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA YA MWAKA 2025**

| | | |
|---|---|---|
| Jina na mwanzo wa kutumika | 1. | Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya (Ushuru wa wa Huduma) ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ya mwaka 2025 na itaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali |
| Eneo la matumizi | 2. | Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Iringa. |
| Tafsiri | 3. | Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:<br><br>"***Afisa Mwidhiniwa***" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.<br><br>"***Halmashauri***" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.<br><br>"***Hesabu***" maana yake ni jumla ya mauzo au manunuzi ikiwa ni pamoja na kodi na ada katika mwaka wa mapato.<br><br>"***Hesabu za mwisho***" maana yake ni taarifa za kihasibu zinazowasilishwa na mlipa ushuru baada ya kipindi cha hesabu kwa mjibu wa kifungu cha 9 cha Sheria Ndogo hizi pamoja na nyaraka au maelezo yatakayotakiwa kutolewa kwa mjibu wa Sheria Ndogo hizi.<br><br>"***Jumuisho***" maana yake ni taarifa, nyaraka, au hesabu au maelezo yoyote yahusuyo kiasi na thamani ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizoanzishwa,zilizosambazwa zilizotolewa na, au kuuzwa kibiashara ikiwa nipamoja na jumuisho la awali au la mwisho.<br><br>"***Kipindi cha hesabu***" maana yake ni muda ambao mfanyabiashara anatakiwa kuwasilisha hesabu za biashara zake.<br><br>***Mkurugenzi***" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa |

| | | |
|---|---|---|
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.<br><br>“***Mwaka wa mapato***” maana yake ni kipindi cha miezi 12 ya Kalenda ya Mwaka.<br><br>***“Mkusanya ushuru”*** maana yake ni mtumishi au wakala aliyeteuliwa na Halmashauri kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria ndogo hizi.<br><br>“***Mlipa Ushuru*** ” maana yake ni mtu binafsi, kampuni au taasisi inayofanya biashara halali au anayetoa huduma katika eneo la Halmashauri.<br><br>***“Sheria”*** maana yake ni Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290<br><br>***“Taasisi ya kibiashara”*** maana yake ni taasisi iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Kampuni au Sheria ya Majina ya Kibiashara inayojihusisha na shughuli za kiuchumi za uzalishaji wa bidhaa za mazao ya Kilimo, usambazaji wa bidhaa au utoaji wa huduma na, au biashara ikiwemo uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi au kikundi au mtu yeyote anayeendesha shughuli za biashara na ana leseni ya biashara<br><br>***“Ushuru wa huduma”*** maana yake ni malipo yanayotolewa kwa Halmashauri kutoka kwa kampuni, tawi la kampuni, mtu au taasisi inayofanya biashara yenye leseni iliyotolewa chini ya sheria yoyote, au kwa huduma za umma inazotumia kufanya biashara katika eneo la Halmashauri.<br><br>***“Wakala”*** maana yake ni mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au taasisi, yoyote iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya ushuru kwa niaba yake.<br><br>***“Waziri”*** maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa. |
| Ushuru wa Huduma | 4. | 1) Halmashauri itatoza ushuru wa huduma kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kutoka kwa kila kampuni, taasisi ya kibiashara au kikundi au mtu binafsi ambaye ana leseni ya biashara katika kila mwaka wa mapato ambayo ni sawa na asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) ya hesabu ya shughuli zote zikiwemo za uzalishaji wa bidhaa au huduma kutoka ndani au nje ya nchi zinazofanyika katika eneo la Halmashauri ukiondoa kodi ya ongezeko la thamani ya mlaji (VAT).<br>2) Ushuru huo utalipwa kwa kuzingatia utaratibu |

RASIMU

| | | |
|---|---|---|
| | | utakaokuwa umewekwa na Halmashauri |
| Uwasilishaji taarifa kuhusu shughuli za kibiashara | **5.** | 1) Itakuwa ni wajibu wa mlipa ushuru yeyote kuwasilisha hesabuzenye taarifa kamili za shughuli za kibiashara zikionyesha thamani ya kiasi na thamani ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizozalishwa, kutolewa, kusambazwa au kuuzwa, kibiashara na taarifa ya fedha katika kipindi maalum kisichozidi siku thelathini (30) tangu tarehe ya taarifa hiyo.<br><br>2) Mkurugenzi kwa taarifa ya maandishi anaweza kumtaka mlipa ushuru yeyote kuwasilisha hesabu zenye taarifa kamili za shughuli za kibiashara zikionyesha thamani ya kiasi na thamani ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizozalishwa, kutolewa, kusambazwa au kuuzwa, kibiashara na taarifa ya fedha katika kipindi maalum kisichozidi siku thelathini (30) tangu tarehe ya taarifa hiyo.<br><br>3) Mkurugenzi anaweza kwa taarifa ya maandishi kumtaka mtu yeyote au taasisi mwenye taarifa au maelezo kuhusu taasisi yoyote ya kibiashara inayopaswa kulipa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, kuwasilisha kwake taarifa au maelezo hayo katika kipindi kisichopungua siku thelathini tangu tarehe ya agizo hilo. |
| Uwezo wa kuingia kwenye jengo | 6. | 1) Mkurugenzi anaweza kumwagiza kwa maandishi Afisa Mwidhiniwa kuingia kwenye jengo au eneo la taasisi ya kibiashara au la mlipa ushuru yeyote kwa nia ya kufanya ukaguzi na tathmini ya kumbukumbu za kibiashara, vitabu vya hesabu, na taarifa nyinginezo kama atakavyoona inafaa kufanyiwa uchunguzi kwa ajili ya kupata na kujua kiwango sahihi cha ushuru anachotakiwa kulipa mlipa ushuru huyo. |
| Wajibu wa mlipa ushuru | **7.** | 1) Kila mlipaji ushuru atatakiwa kutoa au kuwasilisha hesabu za awali za kulipa ushuru unaotakiwa katika kipindi cha wiki ya kwanza ya kila robo mwaka wa mapato.(Januari, Aprili, Julai na Oktoba)<br><br>2) Wafanyabiashara au taasisi au kampuni zinazofanya hesabu zinatakiwa kuwasilisha hesabu zao (financial statement) kabla ya tarehe 31/03 kwa kila mwaka kwa ajili ya kuhakiki na kuoanisha taarifa zilizokwisha kufanyiwa malipo<br><br>3) Kila mfanyabiashara ndani ya halmashauri atatakiwa kujaza fomu maalum inayoonesha 0.3% ya mapato |

| | | |
|---|---|---|
| | | ghafi yake kwa mwaka ambayo italipwa kila robo |
| Kumbukumbu za biashara | **8.** | 1) Mkurugenzi anaweza kwa taarifa ya maandishi kumtaka mlipa ushuru yeyote kuwasilisha kwake kumbukumbu za biashara na vitabu vya hesabu kwa nia ya kupata taarifa kwa ajili ya kufanyiwa tathmini au kukusanya ushuru ndani ya muda utakao ainishwa katika taarifa hiyo. |
| Kiwango cha ushuru | **9.** | 1) Kiwango cha ushuru kitakuwa ni asilimia 0.3% ya hesabu ya shughuli zote baada ya kuondoa kodi ya ongezeko la thamani na kodi ya mlaji.<br><br>2) Bila kuathiri kifungu cha 4(1) cha sheria ndogo hizi; kwa wafanyabiashara wadogo ambao ukokotoaji wa asilimia 0.3% unakuwa mgumu, viwango vya ushuru vitalipwa kwa mujibu wa jedwali la kwanza lililopo katika Sheria Ndogo hizi kulingana na aina na kiwango cha biashara husika.<br><br>3) Iwapo mlipa ushuru hajawasilisha majumuisho ya hesabu zake kwa Mwaka wote wa mapato aidha ametakiwa kufanya hivyo na Mkurugenzi au Afisa mwidhiniwa anafikiri kwamba mlipa kodi huyo ana wajibu wa kulipa kodi kwa mwaka huo anaweza kwa kadri atakavyoona, kuamua kiwango cha hesabu za mlipa kodi huyo isipokuwa tathimini hiyo haitaathiri wajibu wowote wa mlipa kodi anayostahili kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kwa kushindwa kwake kuwasilisha hesabu hizo. |
| Makosa na Adhabu | **10.** | 1) Mtu yeyote au mlipaji yeyote:-<br>(a) Atashindwa kuwasilisha hesabu sahihi kwa wakati;<br>(b) Atashindwa kulipa ushuru kwa wakati;<br>(c) Atashindwa kuwasilisha nyaraka, au taarifa inayotakiwa kuwasilishwa kwa Halmashauri katika muda uliowekwa na Sheria Ndogo hizi;<br>(d) Atashindwa kutunza na kuonesha kumbukumbu kwa Halmashauri kwa ajili ya uchunguzi;<br>(e) Atatoa hesabu za uongo kwa kupunguza au kutoa hesabu zisizokuwa sahihi;<br>(f) Atatoa taarifa isiyokuwa sahihi kuhusu jambo lolote linaloweza kuathiri jukumu lake au la mtu mwingine la kulipa ushuru;<br>(g) Atandaa au kutengeneza au kusababisha kuandaliwa au kutengenezwa kwa vitabu vya uongo vya mahesabu au Makosa;<br>(h) Atamzuia au atajaribu kumzuia Afisa Mwidhiniwa |

RASMU

| | | |
|---|---|---|
| | | kutekelewa majukumu yake aliyopewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi.<br><br>2) Mtu yeyote ambaye atatenda kosa lolote litakaloashiria kukaidi kutekeleza au kukiuka Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosana ikithibitika na kupatikana na hatia atalazimika kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi Milioni moja (1,000,000/=) au kifungo cha miezi 12 jela au adhabu zote mbili kwa pamoja faini na kifungo na kulipa kodi hiyo anayodaiwa na gharama zote ambazo Halmashauri itaingia katika ufuatiliaji wa kodi hiyo anayodaiwa mlipaji.<br><br>3) Ushuru ambao haujalipwa kwa wakati kama ilivyoelezwa kwenye Sheria Ndogo hizi, itatozwa riba ya jumla ya asilimia moja nukta tano (1.5) kwa mwezi au shilingi elfu hamsini kwa mwezi kutegemea kiwango kipi kitakuwa kikubwa na itatakiwa kulipwa na mlipaji.<br><br>4) Riba itakayotozwa katika Sheria Ndogo hizi itachukuliwa kama ushuru unaostahili kulipwa na njia zote za kukusanya kodi na madeni zitatumika kukusanya riba hiyo kama ushuru unaolipwa na mlipaji. |
| Utoaji wa taarifa ya Uongo | **11.** | 1) Mtu yeyote ambaye bila ya sababu za msingi:-<br>a) Akifanya hesabu za uongo kwa kupunguza au kutoa hesabu zisizokuwa sahihi.<br>b) (b)Atatoa taarifa isiyokuwa sahihi kuhusu jambo lolote linaloweza kuathiri jukumu lake au la mtu mwingine la kulipa kodi.<br>c) (c)Ataandaa au kutengeneza au kusababisha kuandaliwa au kutengenezwa kwa vitabu vya uongo vya mahesabu au kumbukumbu.<br>d) (d)Atamzuia au atajaribu kumzuia Afisa mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake aliyopewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa. |
| Kufifilisha kosa | **12** | 1) Bila kuathiri kifungu cha 11 hapo juu, Mkurugenzi anaweza kumtoza faini mtu yeyote anayedaiwa na Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii ikiwa mdaiwa |

RASMU

| | | |
|---|---|---|
| | | huyo amekiri kosa kwa maandishi kwa kujaza fomu iliyoambatanishwa kwenye jedwali la pili la Sheria Ndogo hii na kuahidi kuwa atalipa deni analodaiwa pamoja na faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=). |

**JEDWALI LA KWANZA**
***(Limetengenezwa chini ya Kifungu cha 9)***

**SEHEMU A**
**VIWANGO VYA USHURU WA HUDUMA KWA WAFANYABIASHARA**

| NA | AINA YA BIASHARA | KIWANGO CHA USHURU WA HUDUMA KINACHOPASWA KULIPWA KWA MWAKA |
|---|---|---|
| 1. | Wafanyabiashara wanaotumia EFD lakini hawaandai hesabu za mwisho | 0.25% ya malipo ghafi |
| 2. | Wafanyabiashara wa vituo vya mafuta ya Dizeli, Petroli na Mafuta ya Taa | 0.25% ya ripoti kutoka EFD inayotumika |
| 3. | Wafanyabiashara wanaotumia EFD lakini wanafunga hesabu zao za mwisho wa mwaka | 0.25% ya mapato ghafi yao kwa mwaka |

**SEHEMU B**
**USHURU WA HUDUMA ZINAZOTOLEWA KATIKA HALMASHAURI**

| NA | AINA YA HUDUMA | KIWANGO CHA ADA NA USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Huduma zinazotolewa na wazabuni, kandarasi, kampuni/tawi la kampuni, duka na watu binafsi wanaofanya biashara katika eneo la Halmashauri | 0.25% ya mapato ghafi katika kipindi husika |
| 2. | Huduma zitolewazo na mawakala na au Taasisi za huduma za kifedha. | 2% ya interest income katika kipindi husika. |

RASIMU

**JEDWALI LA PILI**

*(Imetengenezwa chini ya Kifungu cha 12)*

**FOMU YA KUFIFILISHA KOSA**

Mimi …………………………………………………nakiri mbele ya……… ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri yaWilaya ya Iringa, kwamba, mnamo tarehe ……. ya Mwezi …… Mwaka … nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Kifungu cha ………… cha Sheria Ndogo za (Kodi ya Huduma) za Halmashauri ya Wilaya ya Iringa za Mwaka 2025.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, kwa hiyariyangu niko tayari kulipa kiasi cha Ada/Ushuru unaodaiwa pamoja na faini.

**NATHIBITISHA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARIYANGU NA UFAHAMU WANGU**

Leo tarehe …… mwezi …………… mwaka …………
Jina……………………..…………………………
Saini……………………………………………..

MBELE YANGU:
Jina…………………………………………………
Cheo ………………………………………………..
Saini ………………………………………………
Tarehe………………………………………………

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri yaWilaya ya Iringa uliofanyika tarehe …….Mwezi……. Mwaka 2025 na kushuhudiwa lakiri hiyo ikibandikwa mbele ya:-

…………………………
**ROBERT MASUNYA**
Mkurugenzi Mtendaji,
**Halmashauri ya Wilaya ya Iringa**

………………………
**STEPHEN MHAPA**
Mwenyekiti,
**Halmashauri ya Wilaya ya Iringa**

NAKUBALI……………………
**MOHAMED MCHENGERWA (MB)**
**Waziri wa Nchi OR- TAMISEMI**



RASIMU